Ombi la Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Tabora (Tabora Urban Water Supply and Sewerage Authority - TUWASA) la kurekebisha Bei ya Huduma ya Majisafi na Majitaka lililowasilishwa Tarehe 20 Aprili 2009

(**AGIZO Na. 09-009)**

Tarehe 20 Aprili 2009, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma ya Nishati na Maji (EWURA) ilipokea ombi la Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Mjini Tabora (TUWASA) la kutaka kurekebisha bei za huduma ya majisafi na majitaka. Katika ombi hilo, TUWASA iliomba kuongeza wastani wa bei ya majisafi kutoka Shilingi 500 hadi Shilingi 887.55 kwa mita ya ujazo kwa wateja wa maji safi, sawa na asilimia 77.5. TUWASA iliomba pia kuongeza bei ya majitaka kwa kati ya asilimia 20% na asilimia 230%. TUWASA ilipendekeza pia kuongeza gharama nyingine kwa asilimia kati ya 25% na 100% na kuanzisha gharama mpya zikiwemo gharama za kumhudumia mteja, ada ya kukodisha mita, gharama za uharibifu wa mita na riba kwa deni la maji lililozidi siku 60. TUWASA iliomba kuanza kutumia bei hizo mpya mara baada ya kupitishwa na Bodi ya EWURA.

Pendekezo la bei la TUWASA linalenga kuiwezesha TUWASA kumudu ongezeko la gharama na kuweza kulipia gharama zote za uendeshaji.

Sheria ya EWURA, "Energy and Water Utilities Regulatory Authority Act" (Sura ya 414)", imeipa EWURA uwezo wa kisheria wa kudhibiti marekebisho ya bei katika sekta ya majisafi na majitaka. Katika kutathmini maombi ya TUWASA, EWURA imezingatia, pamoja na mambo mengine, taarifa mbalimbali zilizowasilishwa na TUWASA kama zinavyoelekezwa na mwongozo wa EWURA wa maombi ya kurekebisha bei, taarifa za nyongeza kwa ajili ya kutoa ufafanuzi, hoja na fafanuzi mbalimbali kutoka kwa wadau.

Mkutano wa taftishi ulifanyika tarehe 4 Juni 2009 katika ukumbi wa “Students Centre” mjini Tabora ili kupata maoni kuhusu uhalali wa ombi hilo la kuongeza bei za majisafi na majtaka.

Katika mkutano huo, wadau mbalimbali miongoni mwao wakiwa in Baraza la Watumiaji Huduma zinazodhibitiwa na EWURA (CCC), Baraza la Ushauri la Serikali (GCC), na wananchi wa Tabora walipewa fursa ya kutoa maoni yao kuhusu ombi la TUWASA la kuongeza bei ya huduma zake. Mabaraza yote mawili pamoja na watumia maji walikuwa na hoja kuhusu ubora wa huduma ya maji inayotolewa na TUWASA na uchakavu wa mtandao wa usambazaji maji unaosababisha upungufu wa maji. Pia, Mabaraza ya GCC na CCC walikuwa na hoja juu ya ufanisi hafifu wa TUWASA katika ukusanyaji wa maduhuli, hali iliyosababisha kuwa na deni kubwa la maji ambalo hawajalipwa.

Kufuatia kukamilika kwa taftishi, EWURA imefikia uamuzi kwamba ombi la ongezeko la bei lina mantiki na ni halali isipokuwa makisio ya mahitaji ya fedha yaliyokisiwa pungufu kutokana na kutojumuisha mapato yatokanayo na huduma nyinginezo , kiwango kidogo cha makisio ya maji yatakayozalishwa na mapendekezo ya baadhi ya ada ambazo zinapaswa kulipishwa kulingana na sheria ya maji...

Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA katika kikao chake cha tarehe 25 Juni 2009 ilijadili ombi la TUWASA na kutoa maamuzi yafuatayo:

1. Bodi imeidhinisha ongezeko la bei ya majisafi,majitaka na ada nyinginezo kama zinavyoonyeshwa kwenye jedwali Na 1,2,3,4, na 5 hapa chini.

Jedwali Na.1: Bei za Majisafi kwa Wateja Wenye Dira

Aina ya Mteja	**Bei ya Sasa**	**Bei Iliyopendekezwa TZS/Mita ya Ujazo**		**Bei Iliyoidhinishwa**
	TZS/Mita ya Ujazo.	**Mita za Ujazo**	**TZS/Mita ya Ujazo**	**TZS/Mita ya Ujazo**
Majumbani	500	1-10	600	540
		10 -15	700	630
		Zaidi ya 15	800	720
Taasisi	650	1-15	700	630
		Zaidi ya 15	750	670
Biashara	1,200	1-15	1,000	900
		Zaidi ya 15	1,300	1170
Viwanda	1,300	1-20	1,300	1170
		Zaidi ya 20	1,400	1260
Magati	500		1000	600
Mirambo Barracks	585	1-15	700	630
		Zaidi ya 15	750	670

Jedwali. Na.2: Bei za Majisafi kwa Wateja Wasio na Dira

Aina ya Mteja	**Bei ya Sasa**	**Bei Iliyopendekezwa**	**Bei Iliyoidhinishwa**
	TZS/ Mwezi	**TZS/ Mwezi**	**TZS / Mwezi**
Majumbani	10,000	12,000	12,000
Taasisi	20,000	25,000	25,000
Biashara	25,000	25,000	25,000
Viwanda	30,000	30,000	30,000

Jedwali. Na.3: Bei za Majitaka

Aina ya Mteja	**Mita za Ujazo/Bei kwa Mwezi**	**Bei ya Sasa (TZS)**	**Bei Iliyopendekezwa (TZS)**	**Bei Iliyoidhinishwa (TZS)**
Majumbani	1 - 20 (TZS /Mwezi)	1,200	3,000	3,000
	Zaidi ya 20 (TZS/ m^3)	100	200	200
	Kwa wasio na Mita (TZS /Mwezi)	1,500	5,000	5,000
Taasisi	1 - 20 (TZS /Mwezi)	10,000	15,000	15,000
	Zaidi ya 20 (TZS / m^3)	200	500	500
	Kwa wasio na Mita (TZS /Mwezi)	15,000	25,000	25,000
Biashara	1 - 20 (TZS /Mwezi)	12,000	15,000	15,000
	Zaidi ya 20 (TZS / m^3)	300	500	500
	Kwa wasio na Mita (TZS /Mwezi)	20,000	25,000	25,000
Viwanda	1 - 20 (TZS /Mwezi)	15,000	18,000	18,000
	Zaidi ya 20 (TZS/ m3)	300	500	500
	Kwa wasio na Mita (TZS /Mwezi)	20,000	25,000	25,000
Umwagaji wa Majitaka kwa kila safari (6m3).	TZS/Kila Safari	2,000	5,000	5,000

Jedwali Na. 4: Ada ya Huduma Mbali Mbali

Aina ya Mteja	Maunganisho Mapya ya Maji			Kurejeshewa Huduma			Kuunga Maji isivyo Halali		
	Ada ya Sasa (TZS)	Ada Iliyopend-ekezwa (TZS)	Ada Iliyoidhin-ishwa (TZS)	Ada ya Sasa (TZS)	Ada Iliyopend-ekezwa (TZS)	Ada Iliyoidhin-ishwa (TZS)	Ada ya Sasa (TZS)	Ada Iliyopend-ekezwa* (TZS)	Ada Iliyoidhin-ishwa (TZS)
Majumbani	20,000	30,000	30,000	7,000	10,000	10,000	200,000	250,000	Tumia Kifungu Na. 55 cha Sheria ya Maji na Usafi wa Mazingira ya 2009 (Compounding of offences)
Taasisis	30,000	40,000	40,000	20,000	25,000	25,000	200,000	300,000	
Biashara	30,000	40,000	40,000	20,000	25,000	25,000	200,000	300,000	
Viwandal	60,000	80,000	80,000	60,000	80,000	80,000	200,000	400,000	

*Maji yaliyotumika isivyo halali kuongezwa kwenye ada

Jedwali Na. 5: Ada Mpya za Huduma Mbali Mbali

Aina ya Mteja	Ada ya kutoa Huduma (Service Charge)		Ada ya Kukodisha Mita ya Maji		Malipo kwa Kuharibu Mita ya Maji		Faida KwenyeDeni	
	Ada Iliyopend-ekezwa (TZS)	Ada Iliyoidhin-ishwa (TZS)	Ada Iliyopend-ekezwa (TZS)	Ada Iliyoidhin-ishwa (TZS)	Ada Iliyopend-ekezwa (TZS)	Ada Iliyoidhin-ishwa (TZS)	Asilimia ya Deni lote Iliyopend ekezwa	
Majumbani	3,000	3,000	1,500	1,500	75,000	Kutumia Kifungu Na. 55 cha Sheria ya Maji na Usafi wa	1%	**Haikuidhinishwa**
Taasisi	5,000	5,000	5,000	5,000	120,000		2%	
Biashara	5,000	5,000	5,000	5,000	120,000		2%	
Viwanda	5,000	5,000	5,000	5,000	250,000		2%	

						Mazingira ya 2009 (Compoun -ding of offences		

2. Ifikapo tarehe 30 Septemba 2009 au kabla ya hapo, TUWASA itawasilisha EWURA mpango wake wa:-

   2.1. kufunga mita za maji kwenye kituo cha kusukuma maji cha Igombe ifikapo tarehe 30 Juni 2010;

   2.2. kuendeleza vyanzo vingine vya maji ili kuweza kukidhi mahitaji ya maji kwa siku za usoni; na

   2.3. kuboresha usafishaji wa maji katika kituo cha Kazima.

3. Ifikapo tarehe 30 Septemba 2010, TUWASA itawasilisha EWURA mchanganuo wa matumizi ya fedha kiasi cha TZS 1,107 Millioni zilizotengwa kwa ajili ya uchakavu wa rasilimali za kudumu na rejesho la mtaji, fedha ambazo ni sehemu ya mahitaji ya fedha yaliyoidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya TUWASA kwa mwaka 2009/2010. Matumizi hayo yanatakiwa yahusishe utekelezaji wa miradi ifuatayo;

   (i) kubadilisha kilometa 4 za bomba chakavu, kutengeneza tuta la bwawa la Kazima, kubadilisha ‘electrical frequency convertor’ iliyovunjika na kutengeneza utoro wa bwawa la Igombe;

   (ii) kuchangia jumla ya TZS 315 Millioni kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa maji unaofadhiliwa na SECO unaohusisha unununuzi wa Pampu za maji;

   (iii) kununua na kufunga Mita 800 za maji, kununua na kufunga mfumo wa kompyuta wa kutengeneza bili na kununua na kufunga mtandao wa kompyuta;

   (iv) kujenga Kioski tatu kwenye vitongoji vya Chemchem, Isevya na Kiloleni; na

(v) kulipia gharama ya kuwahamisha wananchi wa Mwinyi na Ipuli iliwapate mahali pakujenga mabwawa ya majitaka.

4. TUWASA inatakiwa kuboresha ufanisi wa kukusanya mapato kutoka wastani wa asilimia 69 kwa mwaka 2008/09 na kufikia wastani wa asilimia 89 kwa mwaka 2009/2010 kama ilivyoanishwa kwenye Mkataba wa Utendaji ("Performance Agreement") kati ya EWURA na TUWASA.

5. Kuongeza ubora wa maji (bacteriological water quality) ili yakidhi viwango vilivyowekwa na Shirika la Afya Duniani (WHO) ifikapo Septemba 2009.

6. Ifikapo au kabla ya tarehe 30 Septemba 2009, TUWASA inatakiwa kuwasilisha EWURA uthibitisho kuwa inatunza rekodi za uzalishaji maji, muda wa kusukuma maji na matumizi ya umeme; na kwamba rekodi hizo zinatumiwa na TUWASA katika mipango yake ya kuongeza ufanisi.

7. TUWASA itaendelea kuwasilisha EWURA taarifa zake za fedha na utendaji kwa mujibu wa mwongozo wa EWURA. Taarifa hizo zitatumiwa na EWURA kutathmini utendaji wa TUWASA ikilinganishwa na asasi zingine zinazotoa huduma za majisafi na majitaka na uboreshaji wa huduma zake. EWURA itazingatia tathmini hii katika kufanya maamuzi ya maombi yote yatakayowasilishwa na TUWASA katika siku zijazo. Inasisitizwa kuwa, TUWASA itaboresha taarifa zote zinazowasilishwa EWURA kila mwezi.

Agizo hili litaanza kutumika kuanzia tarehe 1 Julai 2009.

Simon F. Sayore Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi EWURA		Haruna Masebu Mkurugenzi Mkuu EWURA

Dar-es-Salaam 25 Juni 2009